



**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 26 Mei, 2021.**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua itasomwa.

**I. TAARIFA YA SPIKA:**

**II. MASWALI:**

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

155. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Kutokana na hali ya maisha kuwa ngumu akina mama wengi wamejiajiri katika kazi mbali mbali ikiwemo mama lishe. Hata hivyo mama lishe wamekuwa wakikabiliana na changamoto za ugumu wa biashara zao kutokana na utitiri wa tozo mbali mbali za Halmashauri, Manispaa na Mabaraza ya Miji.

Je, katika kuwasaidia mama lishe kumudu kufanya biashara na kukidhi maisha yao, kwanini Serikali isiweke kiwango kidogo maalumu cha tozo kwa mwaka ambacho hakitaleta uzito kwa akina mama hao kufanya biashara zao.

### **Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

174. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi)  
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,  
Fedha na Mipango:

Pato la Zanzibar linatokana na mapato yatokanayo na kodi ambapo miongoni mwa walipa kodi hao ni wafanyabiashara.

(a) Je, kuna wafanyabiashara wangapi wa Zanzibar wanaochangia pato hilo.

(b) Je, ni kiasi gani kinakusanywa kupitia wafanyabiashara hao.

### **Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

119. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji

Kwa mujibu wa Sheria na muongozo wa Sera ya ajira, kila mfanyakazi anapaswa kulipwa angalau kiasi cha fedha kitakachoweza kumsaidia kimaisha. Hata hivyo, yapo malalamiko ya walinzi wa kampuni binafsi ambao wanalipwa kiasi cha shilingi 180,000 za Tanzania.

(a) Je, Unaweza kutuambia sababu kuu ya waajiriwa hawa kulipwa kima kidogo cha chini cha mshahara.

(b) Je, utalitatuaje tatizo hili la malipo ya baadhi ya wafanyakazi wanaolipwa kiasi kidogo cha fedha.

### **Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

169. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni miongoni mwa Wizara ambazo ni tegemeo kubwa kwa Serikali na wananchi kwa ujumla. Miongoni mwa majukumu yake ni kushughulikia masuala ya uvuvi nchini.

(a) Je, Serikali kupitia Wizara hii imejipanga vipi katika kuwanufaisha wavuvi wadogo wadogo.

- (b) Kwa kuwa Zanzibar tumezungukwa na bahari na wavuvi wengi hawatamii uvuvi wa kisasa kutokana na ukosefu wa vitendea kazi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wavuvi wetu ili waweze kuwa wa kisasa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

47. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika miaka ya hivi karibuni uwekezaji katika sekta ya elimu umekuwa mkubwa kwa baadhi ya wazalendo na wageni kuwekeza katika uanzishaji wa skuli za msingi na sekondari. Hata hivyo, pamoja na kuwa uwekezaji huo ni mzuri kumekuwa na malalamiko makubwa ya wazazi na wananchi kwa ujumla juu ya bei kubwa ya ada zinazotowwa na skuli binafsi.

- (a) Kwa kuwa Serikali ina wajibu wa kuwalinda wananchi wake, Je, ina mpango gani wa kuweka bei elekezi kwa skuli hizo binafsi.
- (b) Kwa nini wakaguzi wa elimu wa Wizara yako, hawaendi kufanya ukaguzi katika skuli hizo binafsi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

199. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ili kuikuza sekta ya michezo katika nchi yetu, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ichukue jitihada ya kuvipitia vilabu vya michezo Wilayani, kwani vinaonekana vimepunguza kasi ya kuendesha michezo ya aina zote.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuzitembelea Wilaya hizo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

13. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji , Maliasili na Mifugo:

Kwa kuwa wakulima wengi wa mazao ya biashara na chakula katika vijiji mbali mbali hapa Unguja na Pemba hulazimika kupata mazao machache kutokana na kuendeleza kilimo cha asili na kutotumia mbegu bora za kisasa.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani endelevu wa kutoa taaluma kwa wakulima hao.
- (b) Ni lini Serikali itawapelekea wakulima hao mbegu chotara (hybrid) zenye uwezo wa kutoa mazao mengi katika eneo dogo la kilimo.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2021/2022.

Zanzibar,  
26 Mei, 2021.

**(Raya Issa Msellem)**  
**KATIBU WA BARAZA**